# Maelezo ya Kutuma Maombi ya Kujiunga na Programu kwenye Tovuti

### Tuma maombi kwa Programu ya Viongozi Chipukizi: Toleo la Afrika Mashariki

---

Programu ya Viongozi Chipukizi ya Shirika la Women Deliver [Toleo la Kiswahili] [Toleo la Kifaransa] [Toleo la Kinyarwanda ] ni programu ya uongozi inayochukua miaka miwili. Programu hii inawasaidia wanaharakati vijana walio na hamu ya kuleta mabadiliko kwa kuwapa rasilimali, majukwaa, miunganisho, na mafunzo wanayohitaji ili kupanua na kufikia malengo yao ya utetezi." Women Deliver, shirika ambalo limetoa ahadi thabiti ya kushughulikia masuala ya usawa wa kijinsia na afya na haki za ujinsia na uzazi (SRHR), na lina historia thabiti yaushiriki wa vijana unaozingatia usawa na uongozi wa pamoja.

Programu ya Viongozi Chipukizi (Emerging Leaders) ni programu yenye lengo maalumu, iliyo na rasilimali za kutosha na inayoshughulikia mada maalumu zitakazoshirikisha safari ya utetezi ya kila mojawapo wa Kiongozi Chipukizi (Emerging Leader). Programu hii ni tokeo la hatua zetu za:

- Kukadiria kazi za shirika letu za mwongo mmoja wa mafunzo yenye thamani tuliyoyapata
- Kutafakari kuhusu mageuzi yetu wenyewe kama shirika
- Kufanya mashauriano mengi na vijana na washirika nyanjani

Shirika la Women Deliver litafanya kazi na kila Kiongozi Chipukizi katika kuendeleza safari yake kupitia ufadhili, msaada, mafunzo, na rasilimali.

**Je, Ni Nani Anayestahiki Kushiriki katika Programu hii?**

Vijana (wenye umri wa miaka 15-29) wa jinsi na utambulisho wowote wa kijinsia ambao:

- Wanaishi na kufanya kazi nchini Burundi, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Tanzania, na Uganda
- Wanatetea afya na haki za ujinsia na uzazi (SRHR) na/au usawa wa kijinsia, hasa utetezi unaolenga wasichana waliobalehe wanaopatikana katika jamii zao. Upendeleo utatolewa kwa vijana walio na uzoefu na wanaovutiwa na mada tunazolenga za: huduma ya afya kwa wote, haki na usawa katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi, na hatua za kupambana na harakati zinazopinga haki za afya ya ujinsia na uzazi.

[TUMA MAOMBI YA KUWA KIONGOZI CHIPUKIZI LEO]

**Maombi yatafungwa tarehe 30 Mei 2024, saa 11:59 Usiku, (23:59) Saa za Afrika Mashariki**

**Cha Mwongozo wa Kutuma Maombi:** Unapojaza fomu hii ya maombi, tunapendekeza sana usome mwongozo wa kutuma maombi KABLA ya kuanza kujaza maombi. Hii itaturuhusu kuona maswali kwenye maombi mapema na kutoa maelezo zaidi kuhusu mchakato wa kutuma maombi na vigezo vya uteuzi.

Unaweza kuandaa majibu yako mapema ukiwa nje ya mtandao, na pia unaweza kuhifadhi maombi mtandaoni na uyarejelee baadaye ili ukamilishe na kuyawasilisha.

**Fursa Zinazotolewa na Programu Hii:**

Safari ya kila Kiongozi Chipukizi anayejiunga na Programu ya Viongozi Chipukizi itabinafsishwa kulingana na malengo yake ya utetezi, na vile vile malengo yake ya kujenga na kuimarisha ujuzi wake wa kibinafsi na ukuaji kama mtetezi. Fursa zinazopatikana kwa Viongozi Chipukizi katika safari hii zinajumuisha:

- **Mafunzo, Ushauri, na Mafunzo ya Wanarika:** Programu hii ya Viongozi Chipukizi ina lengo la kuwapa Viongozi Chipukizi ujuzi muhimu wa utetezi na maarifa muhimu ili kufaulu katika jukumu lao kama watetezi, kwa hivyo, itawezesha uzoefu wa kujifunza kwa pamoja. Kulingana na safari za kujifunza zilizobinafsishwa, zilizoundwa kibinafsi, Viongozi Chipukizi watatoa na kupokea mafunzo, kuunda na kupokea rasilimali, kufaidika na ushauri unaofaa kutoka kwa Vijana Viongozi Waliohitimu walio katika eneo au nchi yao, na watapata kushiriki katika fursa za kushiriki maarifa ya rika-kwa-rika.
- **Ufadhili Bora:** Viongozi Chipukizi watapewa ruzuku ya miezi 18, inayonyumbulika, inayotegemea hazina ya kuanzia Dola za Marekani $5,000 - $50,000 ili kuwasaidia katika utetezi wao na kuimarisha mashirika yao, pamoja na usaidizi wa kiufundi na rasilimali mahususi kutegemea muktadha.
- **Kuandaa Mikutano:** Shirika la Women Deliver linajulikana sana kwa uwezo wake wa kuandaa mikutano, na hii itapanuliwa hadi kwa Programu ya Viongozi Chipukizi. Kila Kiongozi Chipukizi atahudhuria **Warsha moja ya Ufunguzi** inayofadhiliwa kikamilifu na **Warsha moja ya Kufunga** inayofadhiliwa kikamilifu, kila mojawapo ya warsha hizi imeundwa ili kujenga uhusiano miongoni mwa Viongozi Chipukizi na kupanua mafunzo yanayotokana na malengo yao ya kujifunza yaliyobinafsishwa. Warsha hizo zitaongozwa na kuundwa kwa pamoja na Viongozi Chipukizi.
- **Mfumo Saidizi wa Ushirikiano na Washirika:** Programu ya Viongozi Chipukizi inazipanua fursa za ufikiaji na ushirikiano wa Viongozi Chipukizi kwa mashirika au mitandao ya kitaifa, kikanda, au kimataifa ya utetezi na kutoa huduma za utetezi, usaidizi na mshikamamo wa wanawake kwa pamoja.
- **Ushiriki wa Kisiasa na Ushawishi katika Nafasi za Utetezi za Kikanda na Kimataifa:** Fursa hizi zinazotambuliwa na Viongozi Chipukizi kama sehemu ya maandalizi ya programu zao za utetezi, ushiriki wa kisiasa na fursa za ushawishi huwaruhusu Viongozi Chipukizi kushirikiana moja kwa moja na watoa maamuzi na waundaji sera. Fursa hizi zinazofadhiliwa kikamilifu zinaweza kujumuisha kujiunga na bodi ya uongozi au ushauri, kuzungumza katika matukio na mikutano husika na ifaayo, au kushiriki katika mikutano na mabaraza ya utetezi wa sera. Viongozi Chipukizi watajenga wasifu wao kama wataalam na viongozi kwa usaidizi wa shirika la Women Deliver, ambalo litatumia uhusiano wake ili kuwapa watetezi uwezo wa kufikia majukumu na nafasi za kufanya maamuzi. Pamoja na hayo, Women Deliver itatumia ushawishi wake katika Global Spaces ili kushinikiza ushirikishaji wa vijana wenye usawa na wa kimaana katika nafasi za kimataifa na kikanda za kufanya maamuzi.

**Ustahiki:**

- **Eneo:** Women Deliver inafuraha kutangaza kwamba kanda ya kwanza ya Programu ya Viongozi Chipukizi itakuwa Afrika Mashariki, hasa vijana wanaoishi na kufanya kazi katika nchi zifuatazo: Burundi, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Tanzania, na Uganda
    - Huhitaji **kuwa raia wa au kutoka nchi hizi** - unahitaji tu kuishi na kufanya utetezi wako katika nchi hizi.
    - **Kighairi Maalumu:** Ikiwa **huishi katika mojawapo ya nchi hizi** (lakini kazi yako ya utetezi bado inalenga mojawapo ya nchi hizi) ***kwa sababu si salama kwako kuishi huko unapofanya kazi yako ya utetezi,*** unastahiki programu hii. Ikiwa hii ndio hali yako, utapewa fursa ya kufafanua hali yako katika maombi.
        - Kwa mfano: Wewe ni mtetezi wa haki za LGBTQIA+ katika mojawapo ya nchi zinazostahiki, lakini unaishi Afrika Kusini kwa kuwa haikuwa salama kwako kuishi katika nchi inayostahiki unapofanya kazi hii.
- **Umri:** Wanaotuma maombi ya kujiunga na programu hii lazima wawe na umri wa kati ya: miaka 15-29 kuanzia tarehe 1 Oktoba 2024. Ikiwa una umri chini ya 18, utahitaji ruhusa na idhini kutoka kwa mzazi/mlezi wako ili kujiunga na programu hii.
- **Jinsia:** Programu hii iko wazi kwa utambulisho wote wa kijinsia kukiwa na msisitizo kwa wale wanaojitambulisha kuwa wasichana, wanawake, au wasiojitambulisha kwa jinsia yoyote.
- **Utetezi:** Mtuma maombi ya kujiunga na programu lazima awe mtetezi wa afya na haki za ujinsia na uzazi (SRHR) na/au usawa wa kijinsia, hasa utetezi unaolenga wasichana waliobalehe wanaopatikana katika jamii yake. Upendeleo utatolewa kwa vijana walio na uzoefu na wanaovutiwa na mada tunazolenga za: huduma ya afya kwa wote, haki na usawa katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi, na hatua za kupambana na harakati zinazopinga haki za afya ya ujinsia na uzazi.
    - **Mpango wa Afya kwa Wote (UHC)**: Mpango wa Afya kwa Wote (UHC) unamaanisha kuwa huduma bora za afya zinapatikana kwa kila mtu bila mzigo wa kifedha. Ingawa UHC inahusisha huduma mbalimbali za afya, ni muhimu kuyapa kipaumbele mahitaji ya afya ya wasichana na wanawake, hasa afya na haki zao za ujinsia na uzazi (SRHR), ili kufanya UHC na huduma za ulinzi wa afya kwa wote kuwa halisi na za kweli.
    - **Haki na Usawa katika Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi:** Janga la mabadiliko ya tabiachi duniani linaathiri vibaya wale ambao wamechangia kwa uchache zaidi: wasichana waliobalehe, wanawake, na watu wa jinsia tofauti tofauti. Kundi hili la watu lina rasilimali chache zaidi za kustahimili na kupata nafuu katika mishtuko na mifadhaiko ya tabianchi, na wanakundi hili wanabeba mzigo mkubwa kutokana na mikakati ya kijamii na ya nyumbani ya kukabiliana na janga hili .
    - **Kupambana na Harakati Zinazopinga Haki za Afya ya Ujinsia na Uzazi:** Kwa miongo kadhaa, kumekuwa na muungano unaoendelea kukua na unaofadhiliwa vyema wa watetezi wanaopinga juhudi za afya na haki za ujinsia na uzazi; na ambao wametoa changamoto na kutaka kuangamiza uhuru wa kimwili wa wasichana na wanawake na afya na haki za ujinsia na uzazi (SRHR). Angalau dola za Marekani bilioni $1 zimetumwa ulimwenguni kote kuunga mkono harakati za kupinga afya na haki za ujinsia. Ushawishi wao unaokua unadhihirika wazi katika sera mbalimbali zinazodidimizwa katika ngazi ya kitaifa. Pia wamejipenyeza kimkakati katika majukwaa katika ngazi ya kimataifa ili

kuendesha na kutumia lugha ya maneno makali dhidi ya haki za kibinadamu na kukandamiza sauti zinazounga mkono afya na haki za ujinsia na uzazi (SRHR) ndani ya mashirika ya kiraia.

- **Kanuni za Maadili:** Ili kujiunga na programu hii, ni lazima ukubaliane na kanuni za maadili za shirika letu, zilizounganishwa hapa [Toleo la Kiswahili]. Zaidi ya hayo, Viongozi wote Chipukizi watalindwa na lazima wakubali kuzingatia Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto na Vijana ya Women Deliver [Toleo la Kiswahili].
- **Lugha:** Programu hii inahitaji umahiri katika lugha ya Kiingereza. Women Deliver inachukua hatua za kupanua mipangilio ya programu ya baadaye kuwa katika lugha nyingi. Ikiwa una umri wa chini ya miaka 18 au ungependa kushiriki maelezo kuhusu programu hii na walio katika familia au jamii yako ambao hawazungumzi Kiingereza, tumetafsiri hati zifuatazo katika Kiswahili, Kifaransa, Kinyarwanda:
    - Wavuti: Viongozi Chipukizi kwa Ajili ya Mabadiliko [Toleo la Kiswahili]
    - Kanuni ya Maadili ya Programu ya Viongozi Chipukizi [Toleo la Kiswahili]
    - Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto na Vijana ya Women Deliver [Toleo la Kiswahili]
- **Uwepo wa Intaneti:** Shughuli za programu zitafanyika mtandaoni, hata hivyo, baadhi ya shughuli, kama vile warsha za ufunguzi na kufunga, zitakuwa za moja kwa moja. Women Deliver ina furaha kutoa marupurupu ya data na/au malipo ya vifaa ili kusaidia Viongozi Chipukizi kufikia intaneti kwa ajili ya shughuli za programu.
- **Ushiriki Kamili:** Ili kunufaika zaidi na programu hii, Viongozi Chipukizi wanapaswa kuwa watetezi waliojitolea na wenye shauku ya kuleta mabadiliko; walio tayari kushiriki kikamilifu katika shughuli za programu, na wanaopenda kutenga muda muhimu kwa miradi yao wenyewe ya utetezi. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu jinsi programu hii inavyokufaa, tafadhali tazama mwongozo huu wa ushiriki.

**Maswali yoyote kuhusu ustahiki wako?** Baruapepe" ELP-App@womendeliver.org

## Muda wa Kupata Mshindi

- **15 Aprili 2024:** Kutuma maombi ya kujiunga na **Programu hii ya Viongozi Chipukizi ya 2024: Toleo la Afrika Mashariki** litafunguliwa saa 12:00 usiku Saa ya Afrika Mashariki (EAT)**.**
- **Aprili – Mei 2024:** Women Deliver wataandaa vipindi viwili vya maelezo kuhusu Programu ya Viongozi Chipukizi. Ikiwa una nia ya kujiunga na vipindi, unaweza kujiandikisha kwa ajili ya vipindi hivi hapa chini. Ikiwa huwezi kuhudhuria, bado unaweza kujiandikisha kwa mojawapo na rekodi itatumwa kwa akaunti yako.
    - **Aprili 29 saa 4:00 – 6:00 jioni** Saa za Afrika Mashariki (Jiandikishe hapa)
    - **Mei 15** saa **4:00 – 6:00 jioni** Saa za Afrika Mashariki(Jiandikishe hapa)
- **Mei 30, 2024**: Kipindi cha kutuma maombi kwa **Kundi la Viongozi Chipukizi la 2024 la Afrika Mashariki** kitafungwa saa 11:59 Usiku (11:59) Saa za Afrika Mashariki. Bonyeza hapa ili kukumbushwa siku tatu kabla ya kufungwa kwa maombi.
- **Juni – Julai 2024:** Maombi yanakaguliwa na kamati yenye watu tofauti tofauti inayoundwa na wafanyakazi wa Women Deliver, Viongozi Vijana Waliohitimu, na mashirika bia yenye utaalamu

wa kina wa mada na kikanda na kieneo. Kati ya maombi yote yaliyowasilishwa, takriban wafuzu 60 wa nusu fainali watachaguliwa kwa awamu inayofuata.

- **Mwisho wa Julai 2024:** Watuma maombi ya kujiunga na programu watajulishwa ikiwa wamechaguliwa kama wafuzu katika nusu fainali au la. Ikiwa umechaguliwa kama mshindi wa nusu fainali, utaalikwa kujipanga kwa mahojiano ya kikundi, hii ni hatua ya mwisho ya mchakato wa kutuma maombi.
- **Agosti 2024:** Mahojiano ya vikundi yatafanywa na waliofika katika awamu ya nusu fainali.
- **Mwishoni mwa Agosti 2024:** Uteuzi wa mwisho utafanywa, na wote waliofuzu katika nusu fainali watajulishwa ikiwa wameteuliwa au la.
- **Septemba 2024:** Kujiunga na Programu ya Viongozi Chipukizi kunaanza, ikijumuisha wito wa kukaribishwa. Viongozi Chipukizi wataombwa kushiriki habari zitakazotumika katika tangazo la kundi jipya la Viongozi Chipukizi na kuongezwa kwenye tovuti ya Women Deliver.
- **Oktoba 1, 2024:** Kuanza rasmi kwa Programu ya Viongozi Chipukizi kwa Ajili Mabadiliko.

**Kuhusu Programu ya Viongozi Chipukizi:**

- **Malengo ya Programu:**
  - **Ujuzi, chapa/wasifu ulioimarishwa, na rasilimali zilizoimarishwa za Viongozi Chipukizi** ili kuendeleza na kutekeleza miradi yao ya utetezi inayohusiana na SRHR, hasa kwa wasichana waliobalehe katika miktadha yao.
  - **Uhusiano ulioimarishwa kati ya sauti zilizopuuzwa kutoka jadi, kama vile Viongozi Chipukizi na watoa maamuzi wenye uwezo wa** kushawishi sera za kisiasa na kifedha.
  - **Kuongezeka kwa fursa za kushiriki katika mikutano ya kimataifa ili kujenga maridhiano na kukuza ushirikiano thabiti,** miongoni mwa washirika wasiotarajiwa, wakiwemo Viongozi Chipukizi na watoa maamuzi.
  - **Vuguvugu la Viongozi Chipukizi wenye ari, Viongozi Vijana Waliohitimu na watetezi wa vijana** ili kuendeleza SRHR katika miktadha yao husika na ya kitaifa na katika nafasi za kimataifa ili kuwafanya watoa maamuzi kuwajibika.
- **Muundo wa Kulenga Eneo Moja la Kikanda:** Women Deliver watalenga eneo moja kwa wakati mmoja, wakiwapa Viongozi Chipukizi kutoka eneo hilo usaidizi ulioratibiwa, wa kuzingatia muktadha mahususi na utaalamu wa maeneo yao husika. Pindi tu kikundi kitakapoanza na kuendelea na shughuli za programu, Women Deliver itaanza mchakato mwingine wa kuwatafuta vijana chipukizi katika eneo lingine, na mengineyo. Madhumuni ya kuangazia maeneo kwa wakati mmoja, badala ya yote kwa wakati mmoja, ni kuunda na kukuza hisia za jamii, muunganisho, na kujenga muungano miongoni mwa Viongozi Chipukizi kutoka eneo hilo.
- **Msaada wa Pamoja: :** Ili kutoa usaidizi thabiti wa mtu binafsi kwa kila Kiongozi Chipukizi, ukubwa wa kundi kwa kila eneo utatofautiana kutoka kwa watu 30-50 ambao watapata fursa ya kufanya kazi kwa ushirikiano. Hii itahakikisha kila mtu anapata usaidizi anaohitaji ili kutekeleza utetezi wake kwa ufanisi.
- **Mtazamo Mpya Unaolenga Wasichana Waliobalehe:** Mwanzo wa ujana kwa wasichana unawakilisha hatua ya mtengano ambapo uhuru wao wa kimwili huanza kuwekewa vikwazo,

kutiliwa shaka, na kudhibitiwa. Kwa kulenga sehemu hii ya mchepuko - na sababu zinazochangia hilo - Viongozi Chipukizi watafanya kazi ya kushughulikia suala hili katika hatua hii ya ukaguzi.

- **Kutoa Mtazamo Thabiti kwa Kushughulikia Mada Mahususi:** Huku kazi za Viongozi Chipukizi, zikilenga sana SRHR na Usawa wa Kijinsia, zitazingatia masuala yafuatayo: Haki na Usawa katika Masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi, Hatua za Kupambana na Harakati Zinazopinga Haki za Afya ya Ujinsia na uzazi, na Huduma ya Afya kwa Wote.
- **Afya ya Kiakili, Ustawi, na Ulinzi Salama katika Kituo.** Kazi ya watetezi na wanaharakati haina mwisho, na inaweza kuwa yenye gharama. Women Deliver watasaidia afya ya kiakili na kihisia ya Viongozi Chipukizi, huku wakihakikisha kuwa wanasaidiwa wakati wa kila hatua ya safari yao. **Kiungo cha Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto ya Women Deliver.**

---